REPUBLIC OF KENYA
EXECUTIVE OFFICE OF THE PRESIDENT
OFFICE OF THE PRESIDENT'S ADVISOR
ON WOMEN RIGHTS

# HOTUBA YA KUZINDUA WA MPANGO 'EMPOWER HER', KAKAMEGA

**Salamu**

ABSA Bank

African Guarantee Fund

Kenya National Chamber for Commerce and Industry

Serikali ya Kaunti ya Kakamega

Mabibi na mabwana

Habari zenu!

Milembe vosi!

1. Nchini Kenya wanawake hutoa mchango mkubwa kwa uchumi, katika ukuaji wa uchumi na maendeleo. Ushiriki wa wanawake katika Biashara

Ndogo, Ndogo na za wastani ambazo zinaongeza mapato, akiba na michango ya kodi katika ngazi ya familia, jamii na kitaifa.

2. Ajenda ya Serikali ya Bottom-up Economic Transformation plan inazingatia Biashara Ndogo na za Kati (MSMEs) kwa sekta yenye mchango mkubwa kwa uchumi wa nchi. Sekta ya MSMEs imetambuliwa na kupewa kipaumbele kama kigezo muhimu ya kufikia malengo ya mpango wa maendeleo. Hii inatarajiwa kuhakikisha kwamba ukuaji wa uchumi wetu kama taifa unajumuisha wakina mama.

3. Hesabu hazidanganyi! Wanawake ni wengi wanaoendesha biashara ndogo ndogo ambazo zinachangia asilimia hamsini kwa nafasi za kazi na asilimia thelathini kwa Pato la Taifa (GDP). Imetambulika kwamba, Biashara zinazoongozwa na wakina mama zina mchango mkubwa sana kwa uchumi na Maendeleo ya taifa.

4. Serikali imeandaa programu kadhaa za kifedha ili kuwasaidia wanawake kupata mikopo nafuu pamoja na kuongeza wakina mama kuweza kushiriki katika maamuzi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Baadhio ya mipango hii ni Fedha za Hustler, Fedha za Wanawake wa Biashara na Fedha za Uwezo. Serikali ingali itazindua mipango zaidi kama kuanzisha kampuni ya dhamana ya mikopo (Credit Guarantee) ili kuruhusu wanawake zaidi kukopa.

5. Uzinduzi wa Programu ya Kaunti ya "Empower Her" ni dhibitisho la hitaji la kusaidia biashara zinayoongozwa na wanawake. Hii ndiyo sababu Afisi yangu inashirikiana na wadau katika sekta binafsi ili kupanga mipango ambayo inaweza kukufikia wewe kama mama. Hii ndiyo sababu kuu kwa nini Mheshimiwa Rais aliunda ofisi ya Mshauri wa Haki za Wanawake, kuonyesha kujitolea kwake kwa kila mwanamke na msichana wa Kenya.

6. Wakina Mama, mpango tunaozindua leo ni moja ya mambo ya kwanza ambayo mimi nilianza

kufikiria wakati Rais aliniteua. Maswali kadha wa kadha yalitukumba.

- Tunahakikishaje kwamba wakina mama wana pesa za kufanya biashara zao?
- Je, ni nini kinachozuia wakina mama kuendelea na biashara zao?
- Je, tunashirikianaje na mashirika ambayo yanaweza kusaidia wanawake?
- Je, tunawaelimishaje wanawake ili waweze kuwa washindi wa biashara zinazo nawiri?

7. Mradi huu tunaotarajia kuzindua hapa leo ni mwanzo wa kujibu maswali haya. Tumekuja kukuwezesha lakini tunajua kwamba kuna Mungu ambaye amekupea nguvu ndani yako kukusukuma kutimiza ndoto zako.  Je, unajua mfano wa talanta tano kwenye Biblia takatifu?

8. **Katika Mathayo sura ya 25 mstari wa 14 - 30, moja ya mifano muhimu zaidi ya Yesu kuhusu**

**kazi imewekwa katika muktadha wa uwekezaji**. Mtu tajiri awasilisha usimamizi wa mali yake kwa wafanyikazi wake. Akatoa talanta tano kwa mtumishi wa kwanza, talanta mbili kwa wa pili, na talanta moja kwa wa tatu. Leo tunatoa talanta kwa njia ya elimu ya kifedha hapa kwenu. Unachofanya nacho kitatuambia kama wewe ni mtumishi wa kwanza, wa pili au wa tatu katika mfano wa hadhi ya Yesu.

Wakina Mama,

9. Mradi huu uluundwa kuwa mwanzo wa wewe kama mama kuweza kuwa gwiji wa biashara na kuzidisha mapato yako. Kupitia programu hii, utapata ujuzi muhimu katika maeneo kama masomo ya kifedha, maendeleo ya biashara, na uongozi. Wakati wa mafunzo utaweza kujumuika na kuungana na wanawake wengine wenye msukumo, kubadilishiana safari zetu za biashara na kujenga mtandao wenye nguvu wa msaada.

10. Kumbuka, haupewi kuwa na uwezo, inabidii udai. Mradi huu ni chombo, lakini nguvu na msukumo halisi iko ndani yako wewe. Muhimu zaidi, utagundua kwamba nguvu ya sauti yako mwenyewe. Utakuwa na vifaa vya kufutialia ndoto zako, kuvunja vikwazo, na kufikia uwezo wako kamili kama mama.

11. Kama mama, jiwekee maarifa, jipe changamoto na usiogope kuota ndoto kubwa. Fikiria juu ya biashara unayotaka kujenga, mabadiliko unayotaka kufanya na urithi unaotaka kuacha nyuma. **Mithali sura ya Kumi na tatu msitari wa ishirni na mbili unasema**, **"Mtu mwema huacha urithi kwa watoto wa wanawe".** Wakina mama, naamini tuna uwezo wa kufanya mengi kwa ajili yetu wenyewe na familia, kutokana na kupewa uwezo.

12. Una wazo la biashara inayofaa, anza! Na taasisi za kifedha zitakuja kusaidia kwa ufadhili. Kazi yangu ni kuhakikisha kwamba unapata uwezo unaohitaji zinazopatikana ndani ya taifa letu kupitia

washirika kama ABSA Bank na wengine. Kauli mbiu yetu ni kwamba kila mama ni mwanamke bomba na kwa hivyo hakuna anayepaswa kuachwa nyuma.

13. Kumbuka kwamba hivi karibuni Kaunti zitakuwa na Hifadhi za Viwanda (*County Aggregation and Industrial Parks* - CAIPs). Ndoto ya ofisi yangu ni kwamba hizi sehemu za biashara zitajaa wakina mama wa biashara. Sehemu hizi za kukusanya na viwanda zinakusudiwa kuongeza thamana katika bidhaa zinazozalishwa kwenye Kaunti. Baada ya yote, wakina mama ndio wako kwenye mashamba wakilima. Wahenga walisema, **Kidole kimoja hakiui chawa**, kwa hiyo nawasihi tuunde vikundi, tukue kwenye vyama vya ushirika ili tuanze kuendesha uchumi wa kata yenu tunapojiandaa kuchukua hifadhi za Viwanda.

14. Hatua ndogo unazochukua hapa leo zinaashiria mwanzo wa safari ya ya kuwezeshwa kiuchumi. Kumbuka, sisi kama wakina mama ni watu wa msukumo wa mabadiliko. Pamoja, tunaweza

kuandika tena hadithi nzuri kama wakina mama. Tunaweza kuuonyesha ulimwengu nguvu isiyozuilika ya wakina mama wa Kenya ambao wako na uwezo. Leo utajifunza na kisha utawafundisha wakina mama wengine, hii itakuwa na athari kubwa na nzuri katika familia yako, kijiji, kaunti na taifa kwa jumla.

15. Leo tumekusanyika hapa kuanza safari hii ya ajabu ya kuwezesha wa wakina mama na wasichana na uwekezaji kupitia mradii huu wa mafunzo ya "Empower Her".

Je, uko tayari kuwa na uwezo?

Kwa hiyo, hebu tuanze! Hebu “Empower Her” kwa pamoja!

Sasa ni furaha yangu kutangaza Mpango wa “Empower Her” imezinduliwa rasmi!

Asanteni sana!

Mh. Harriette Chiggai

Mshauri wa Rais kuhusu Haki za Wanawake